

 <b>UNIVERSITY of MARYLAND CAPITAL REGION HEALTH</b>		<b>PFS SERA NA UTARATIBU MWONGOZO</b>
<b>Kichwa:</b> Msaada wa Kifedha		<b>Nambari ya Utaratibu:</b> PFS.FIN.01
<b>Mwanzilishi:</b> Huduma za Fedha kwa Mgonjwa	<b>Tarehe ya Kuanzia:</b> 3/2/2017	<b>Tarehe ya Tathmini/Marudio:</b> 3/2/2017
<b>Imeidhinishwa na:</b> Eileen Pride		
<b>A.</b> Msimamizi/Meneja	<b>B.</b> Msaidizi Mkurugenzi wa Idara	<b>C.</b> Bw. Mkurugenzi, Huduma za Usaidizi wa Kifedha kwa Wagonjwa

## SERA:

DHS imejitolea kutoa msaada wa kifedha kwa watu walio na mahitaji ya huduma za afya na hawana bima, hawana bima kamili, hawastahiki kwa mipango ya serikali, au kwa sababu zingine hawawezi kulipia matibabu ya magonjwa yanayojitokeza na yanayohitaji matibabu, kulingana na hali zao binafsi za kifedha.

Ni sera ya Vituo vya DHS kutoa Msaada wa Kifedha kulingana na hali ya umaskini au gharama kubwa ya matibabu kwa wagonjwa ambao wanatimiza vigezo maalum vya kifedha, wanaoomba msaada huo. Madhumuni ya kauli ya sera ifuatayo ni kueleza jinsi maombi ya Msaada wa Kifedha yanapaswa kufanyika, vigezo vya kustahiki, na hatua zinazofanyika katika kuchakata maombi.

Vituo vya DHS vitachapisha maelezo kuhusu upatikanaji wa Misaada ya Kifedha kila mwaka katika magazeti yao ya mitaa na kuweka noti za upatikanaji katika maeneo sahihi pamoja na Ofisi ya Malipo. Noti za upatikanaji pia zitatumwa kwa wagonjwa walio na bili. Noti katika maeneo makuu wanayopitia wagonjwa zitawekwa wazi kwa wote. Karatasi ya Bili ya Mgonjwa na Maelezo ya Msaada wa Kifedha itatolewa kabla ya mgonjwa kuondoka na itapatikana kwa wagonjwa wote watakapohitaji.

Msaada wa Kifedha unaweza kuongezwa wakati mapitio ya hali ya kifedha ya mgonjwa binafsi yamefanywa na kunakiliwa. Hii inapaswa kujumuisha mapitio ya gharama yaliyopo ya matibabu ya mgonjwa (ikiwa ni pamoja na akaunti zozote ambazo zimekuwa na malimbikizo ya madeni isipokuwa akaunti ambazo zimepelekwa mahakamani na hukumu kutolewa) na makadirio yoyote ya gharama za matibabu. Maombi ya Misaada ya Kifedha huweza kutolewa kwa wagonjwa ambao akaunti zao zimewekwa na wakala wa kukusanya madeni na hili huweza kutumika tu kwa akaunti ambazo hazijapata hukumu.

DHS ina haki ya kufanya uamuzi wa uwezo wa mgonjwa kuweza kulipa, kwa hiari yake. Wagonjwa wote wanaotafuta huduma za dharura watahudumiwa bila kujali uwezo wao wa kulipa. Ili kupata huduma kwa matatizo ibuka/ya ghafla, maombi kwa Mpango wa Kuidhinisha Misaada yatakamiliwa, kupokelewa na kufanyiwa utathmini. Hata hivyo, taratibu hizo hazitazuia wagonjwa kupata matibabu.

### **JINSI YA KUSTAHIKI KWA MPANGO**

Ilivyo sawa na mwito wao ya kutoa huduma za afya za kipekee na za hali ya juu na kutetea wale ambao wasio na uwezo wa kulipia huduma muhimu za kiafya, hospitali za DHS zinajitahidi kuhakikisha kuwa uwezo wa kifedha wa watu ambao wanahitaji huduma za afya haziwezi kuwazuia kutafuta au kupokea huduma.

**HALI MAALUM AMBAZO HAZITASHUGHULIKIWA NA BIMA CHINI YA MPANGO WA MSAADA WA KIFEDHA ZINAJUMUISHA:**

**UTARATIBU, Maendelezo**

1. Huduma zinazotolewa na watoa huduma wa afya wasio na uhusiano na hospitali za DHS (k.m, vifaa vya kudumu vya matibabu, huduma za afya za nyumbani)
2. Wagonjwa walio na bima zilizo na mipango au sera ambazo haziruhusu bima hizo kulipia huduma (k.m., HMO, PPO, au Fidia kwa Wafanyakazi), hawastahiki kwa Mpango wa Msaada wa Kifedha.
  - a. Kwa kawaida, Mpango wa Msaada wa Kifedha haupatikani kulipia huduma ambazo zimekataliwa na kampuni ya bima ya mgonjwa; hata hivyo, huduma hizo zinaweza kutolewa kwa kuzingatia hali zilizopo na hatari zilizopo za kiafya.
3. Masalio ambayo hayajalipwa yanayotokana na huduma za mapambo au huduma zisizo muhimu za kiafya
4. Vitu vya matumizi ya kila siku ya mgonjwa
5. Vyakula na malazi ya mgonjwa
6. ***Gharama za kumwona daktari zinazohusiana na tarehe ya huduma hazijumuishwi katika sera ya msaada wa kifedha ya DHS Wagonjwa ambao wanataka kupata msaada wa kifedha inayohusiana na kulipia bili za kumwona daktari lazima wawasiliane na daktari moja kwa moja.***

**Wagonjwa wanaweza kosa kustahiki kwa Msaada wa Kifedha kwa sababu zifuatazo:**

1. Kutotoa hati zinazohitajika au kutoa maelezo yasiyo kamili.
2. Kuwa na bima ya HMO, PPO, Fidia za Wafanyakazi, Medicaid, au mipango mingine ya bima ambayo huwanyima huduma za hospitali kutokana na vikwazo/mipaka ya mpango wa bima.
3. Kushindwa kulipa malipo ya ushirikiano kama inavyohitajika na Mpango wa Msaada wa Kifedha.
4. Kushindwa kumudu malipo ya mipango ya sasa ya DHS .
5. Kushindwa kufanya mipango sahihi ya kulipia gharama za awali unazodaiwa na DHS (pamoja na wagonjwa ambao walielekezwa kwa shirika la nje la kukusanya madeni kwa madeni ya awali)
6. Kukataa kuchunguzwa kwa ajili ya mipango mingine ya msaada iliyofanywa kabla ya kuwasilisha ombi kwa Mpango wa Kutoa Idhini ya kupata Msaada wa Kifedha.
7. Kukataa kutoa taarifa zinazohusiana na madai ya kesi ya dhima inayoendelea
8. Raia wa kigeni wanaosafiri kwenda Marekani kutafuta huduma za matibabu zisizo za lazima au dharura.

Wagonjwa wasiostahiki kwa mpango watatakiwa kulipa masalio yoyote ya gharama yaliyopo na huenda wakawasilishwa kwa huduma ya madeni yaliyolimvikizwa ikiwa masalio hayatalipwa katika wakati uliokubaliwa.

Wagonjwa ambao wanaonyesha kwamba hawana ajira wala bima watatakiwa kuwasilisha Maombi ya Msaada wa Kifedha isipokuwa kama wanakidhi vigezo vya Matazamio ya Ustahiki wa Msaada wa Kifedha. Kama mgonjwa amefaulu kupata bima ya COBRA, uwezo wa mgonjwa kuweza kulipa malipo ya bima ya COBRA utapitiwa upya na Mshauri wa Kifedha/Mratibu na mapendekezo yatafanywa kwa Viongozi Wakuu. Watu walio na uwezo wa kifedha wa kununua bima za afya watahimizwa kufanya hivyo, kama njia ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya na kwa afya yao binafsi kwa ujumla.

Kiasi cha malipo ya bima kitahesabiwa kulingana na 200-500% ya mapato kama inavyoelezwa na miongozo ya shirikisho la umaskini na inayochapishwa kila mwaka katika Daftari la Shirikisho. Miongozo mipya hutumika mwezi wa kwanza baada ya kuchapishwa.

**Msaada wa Kifedha wa Awali**

Wagonjwa pia wanaweza kustahiki kwa Msaada wa Kifedha wa Awali. Kuna wakati ambapo mgonjwa huweza kuonekana kuwa anastahiki kwa msaada wa kifedha, lakini hakuna fomu ya msaada wa kifedha kwenye faili. Kuna maelezo ya kutosha yalizotolewa na mgonjwa au kutoka kwingine, ambayo yanatoa ushahidi wa kutosha ili kutoa msaada wa kifedha kwa mgonjwa. Iwapo hakuna thibitisho la kuonyesha ustahiki wa mgonjwa kwa msaada wa kifedha, DHS ina haki ya kutumia vyombo vya nje au taarifa katika

**UTARATIBU, Maendelezo**

kubaini makadirio ya kiasi cha mapato ili kubaini ustahiki kwa msaada wa kifedha na uwezekano wa kupunguzwa kwa gharama za huduma. Mara inapobainika, kwa sababu za hali ya asili ya msaada wa awali, msaada wa kifedha unaoweza kuidhinishwa ni wa kufutulia mbali 100% ya salio la akaunti tu. Kustahiki kwa Msaada wa Kifedha wa Awali kutalipia gharama za tarehe mgonjwa aliyohudumiwa tu. Kustahiki kwa msaada wa awali kunaweza kubainishwa kwa hali zote zilizopo za mtu binafsi ambazo zinaweza kujumuisha:

- a. Bima ya Msaada wa Kifedha wa Kununua Madawa ya Matibabu
- b. Bima ya SLMB
- c. Bima ya PAC
- d. Kutokuwa na makazi
- e. Msaada wa Matibabu na Huduma kwa wagonjwa Zinazosimamiwa na Medicaid kwa huduma zinazotolewa katika ER nje ya huduma zinazolipiwa nabima katika programu hizi.
- f. Kiasi cha gharama za matibabu unachofaa kulipia ili kustahiki kwa Msaada wa Matibabu
- g. Kustahiki kwa mipango mingine ya misaada ya jimbo au mtaa
- h. Mgonjwa amefariki na hakuna mali yake yoyote inayojulikana
- i. Wagonjwa ambao wamebainika kukidhi vigezo vya ustahiki vilivyowekwa chini ya mpango wa awali wa State Only Medical Assistance Program
- j. Watu ambao sio raia wa Marekani wanaoonekana kuwa hawastahiki
- k. Huduma za Misaada ya Kifedha kwa Matibabu ambazo hazistahiki kwa wagonjwa wanaostahiki kupokea Misaada ya Kifedha
- l. Wagonjwa wasiotambulika (Akaunti zisizojulikana na ambazo juhudi zote za kuzipata na/au kuzitambua hazijafaulu)
- m. Kufilisika, kwa mujibu wa sheria, kama ilivyowekwa na mahakama ya shirikisho

**Huduma maalum au vigezo ambavyo havistahiki kwa Msaada wa Kifedha wa Awali ni pamoja na:**

- a. Taratibu za kuchagua zisizo za lazima (k.m - Mapambo) hazipo kwenye bima katika mpango.
- b. Wagonjwa wasio na bima waliopata huduma katika Idara ya Dharura kwa kuwasilisha Ombi la Dharura hawatastahiki kwa mpango wa msaada wa kifedha wa awali hadi wakati ambapo mpango wa Maryland Medicaid Psych utakaandikiwa bili.

**TARATIBU**

1. Kuna watu walioteuliwa ambao watakuwa na wajibu wa kuchukua maombi ya Misaada ya Kifedha. Wafanyakazi hawa wanaweza kuwa Washauri wa Kifedha, Waratibu wa Kupokea Fedha za Wagonjwa, Wawakilishi wa Huduma kwa Wateja, n.k.
2. Kila juhudi zinazowezezana zitafanywa ili kutoa idhini ya fedha kabla ya tarehe ya huduma. Ikiwa inawezekana, wafanyakazi walioteuliwa watashauriana na wagonjwa waliotuma maombi ya Misaada ya Kifedha kupitia simu au kukutana ana kwa ana wagonjwa ili kubaini kama wanakidhi vigezo vya msingi vya kupata msaada.
  - a. Wafanyakazi watakamilisha uchunguzi wa ustahiki kwa mpango wa Medicaid kwa wagonjwa wa Malipo Binafsi ili kuthibitisha kama mgonjwa ana bima kwa wakati huo.

**UTARATIBU, Maendelezo**

- b. Data za msingi zitaingizwa katika mfumo wa data ya mtu wa tatu ili kubaini uwezekano wa kustahiki. Ili kuwezesha mchakato huu, kila anayetuma ombi lazima atoe maelezo kuhusu ukubwa na mapato ya familia yake. Ili kuwasaidia waombaji kukamilisha mchakato, tutatoa fomu ya maombi ambayo itawajulisha hati zinazohitajika ili kutoa uamuzi wa mwisho wa ustahiki.
  - c. Maombi yalioanzishwa na mgonjwa yatafuatiliwa, kushugulikiwa na uamuzi wa kubaini ustahiki ufanyike ndani ya data ya mtu wa tatu na vyombo vya taratibu hiyo. Barua ya uamuzi wa mwisho itawasilishwa kwa kila mgonjwa ambaye ametuma ombi rasmi la msaada wa kifedha. Kubainishwa kwa Uwezekano wa Kustahiki kutafanywa katika siku mbili za kazi baada ya kuwasilishwa kwa ombi la mgonjwa ili kupata huduma za matibabu bila malipo au kwa bei nafuu, ombi la msaada wa kifedha kwa matibabu, au yote mawili
  - d. Baada ya kupokelewa kwa ombi la mgonjwa, atakuwa na siku thelathini (30) za kuwasilisha nyaraka zinazohitajika ili kubaini ustahiki. Kama hakuna data itakayopokelewa katika siku 30, barua ya kukataliwa kwa ombi itatumwa kumjulisha kuwa ombi limekataliwa kwa kukosa hati zinazohitajika. Mgonjwa anaweza kuwasilisha ombi lake tena kwenye mpango na kuanzisha kesi mpya kama ratiba ya awali haijazingatiwa. Mchakato wa maombi ya Msaada wa Kifedha utafunguliwa kwa takribani siku 240 baada ya bili ya kwanza kutumwa wakati wa mgonjwa kuruhusiwa kuondoka hospitalini.
  - e. Notiisi binafsi kuhusu sera ya huduma ya msaada ya hospitali itatolewa katika muda kabla ya kulazwa au wakati wa kulazwa kwa kila mtu ambaye anatafuta huduma katika hospitali hiyo.
3. Kutakuwa na mchakato mmoja wa maombi katika vituo vyote vya DHS. Mgonjwa anatakiwa kuwasilisha ombi la Msaada wa Kifedha lililokamilishwa kwa njia ya kunena au kwa maandishi. Aidha, yafuatayo yanaweza kuhitajika:
- a. Nakala ya hivi karibuni zaidi ya matangazo ya kodi ya mapato (kama una mume/mke na hamtatangazi kodi kwa pamoja, ambatisha nakala ya matangazo ya mume/mke wako); thibitisho la mapato ya ulemavu (kama inahitajika) thibitisho la mapato ya usalama wa kijamii (kama inahitajika). Ikiwa huna ajira, thibitisho tosha la kukosa ajira kama vile taarifa kutoka Ofisi ya Bima ya Wasio na Ajira, taarifa kutoka kwa mfadhili wa hivi sasa, n.k ...
  - b. Nakala ya hivi karibuni zaidi ya hati ya malipo (kama umeajiriwa) au uthibitisho mwingine wa mapato.
  - c. Ilani ya Kubainisha Msaada wa Kifedha kwa Matibabu (kama inahitajika).
  - d. Nakala za bili ya Rehani au Kodi ya nyumba (kama inahitajika), au nyaraka iliyoandikwa kuhusu hali yako ya sasa ya maisha/hali ya makazi.

Ombi la kuwasilisha maelezo ambayo hayakutolewa yatumwa kwa mgonjwa kwa njia ya maandishi. Kuwasilishwa maelezo yanayohitajika kwa njia ya mdomo kutakubaliwa, panapohitajika.

4. Mgonjwa anaweza kustahiki kupata Msaada wa Kifedha kwa sababu ya ukosefu wa bima ya kamili au kwa kuwa na gharama za juu zaidi za matibabu. Mara baada ya mgonjwa kuwasilisha maelezo yote yanayohitajika, Mshauri wa Kifedha atapitia na kuchambua ombi hilo na kuliwasilisha katika Idara ya Huduma za Kifedha kwa Wagonjwa kwa maamuzi ya mwisho ya ustahiki kulingana na masharti ya DHS.
  - a. Ikiwa ombi la mgonjwa la Msaada wa Fedha limebainika kuwa kamili na sahihi, Mratibu wa Fedha atapendekeza kiwango cha ustahiki wa mgonjwa na kuwasilisha ombi katika idhini ya pili na ya mwisho.
    - i) Kama mgonjwa anastahiki kupata Msaada wa Kifedha, Mratibu wa Fedha atawaarifu wafanyakazi wa kliniki ambao wanaweza kumpangia mgonjwa ratiba ya huduma katika hospitali.

**UTARATIBU, Maendelezo**

- ii) Kama mgonjwa hastahiki kupata Msaada wa Kifedha, Mratibu wa Fedha atawaarifu wafanyakazi wa kliniki kuhusu uamuzi na huduma za hospitali zisizo ibuka/ za dharura hazitapangwa.
  - (1) Uamuzi kuwa mgonjwa huenda akakosa kupangiwa huduma za hospitali, zisizo ibuka/ za dharura unaweza kusikizwa tena na Kamati ya Utendaji ya Kuidhinisha Misaada ya Kifedha, ombi linapowasilishwa.
  - (2) Kamati ya Fedha ya Kutoa kibali, ina Msaidizi Mkurugenzi wa PFS, Mkurugenzi Mkuu wa Vipindi vya Mapato, Meneja wa Hatari wa DHS, na CFO.
  - (3) CFO atatia sahihi kuidhinisha msaada yoyote ya zaidi ya \$50,000.
5. Kila idara ya kliniki inaweza kuchagua kuteua baadhi ya taratibu-chaguzi ambazo hazistahiki kwa Misaada ya Fedha.
6. Mara baada ya mgonjwa kuidhinishwa kupokea Msaada wa Kifedha, bima ya Msaada wa Kifedha inaweza kuanza kufanya kazi kutoka mwezi wa uamuzi huo, hadi miaka 3 kabla, na hadi miezi sita (6) ijayo ya kalenda. Hata hivyo, hakuna viwango vilivyowekwa kudhibiti vipindi vya kustahiki kwa Misaada ya Kifedha. Kila kipindi cha ustahiki kitabainishwa kwa kuzingatia hali zote zilizopo. Ikiwa huduma za ziada za afya zitatolewa baada ya kipindi cha idhini, lazima mgonjwa atume ombi tena kwa mpango ili kuidhinishwa. Aidha, mabadiliko kwa mapato ya mgonjwa, mali, gharama au hali ya familia yanatarajiwa kuwasilishwa kwa Idara ya Mpango ya Msaada wa Kifedha. Shughuli zote za Hatua za Makusanyo Zisizo za Zawaida, kama zinavyoelezwa hapa chini, zitasimamishwa mara tu mgonjwa atakapoidhinishwa kupata msaada wa kifedha na salio zozote za matibabu ya mgonjwa zinapolipwa.

*Hatua za Makusanyo Zisizo za Zawaida (ECAs) zinaweza kuchukuliwa kwa akaunti ambazo hazina mgogoro au ambazo hazipo kwenye mipango ya malipo. Isipokuwa katika hali ya kipekee, hatua hizi zitafanywa baada ya siku 120 kutoka siku ya kuwasilishwa kwa bili ya kwanza kwa mgonjwa na itatanguliwa na notisi siku 30 kabla ya kuanzishwa kwa mchakato wa ECA. Mgonjwa atafahamishwa kuhusu upatikanaji wa msaada wa kifedha na ukaguzi wa ustahiki utafanywa kabla ya hatua yoyote kuchukuliwa.*

  - i) *Amri ya kukusanya deni huenda ikatolewa na koti kwa wagonjwa hao.*
  - ii) *Dai la kumiliki linaweza kuwekwa kwa makazi ya msingi na Mahakama. Hospitali haitafanya juhudi za kumiliki makazi ya msingi lakini tunaweza kudumisha msimamo wetu kama mkopeshaji wa kulindwa ikiwa mali kwa njia nyingine inamilikiwa.*
  - iii) *Masalio ya akaunti zilizofungwa zinazoonekana kwenye ripoti ya mikopo au kupendekezwa kwa hukumu/amri ya mahakama ya kukusanya deni yanaweza kufunguliwa upya ikiwa mgonjwa atawasilisha ripoti ya masalio kituoni. Malipo yatasubiriwa kutoka kwa mgonjwa ili kutatua masuala yoyote ya mikopo, hadi kituo kitakapoamua kuwa salio linalofaa kufutiliwa mbali.*
  - iv) *Hatua za Makusanyo Zisizo za Zawaida zinahitaji idhini ya Kamati ya Kuidhinisha Misaada ya Kifedha.*
7. Ikiwa mgonjwa anabainika kuwa hastahiki, juhudi zote za kukusanya malipo au ushirikiano, au asilimia ya salio linalotarajiwa kwa ajili ya huduma yatafanywa kabla ya tarehe ya huduma au inaweza kupangwa kufanyiwa ukusanyaji katika tarehe ya huduma.
8. Barua ya uamuzi wa mwisho itawasilishwa kwa kila mgonjwa ambaye amewasilisha ombi rasmi.

**UTARATIBU, Maendelezo**

9. Maamuzi ya kumrudishia mgonjwa pesa yanafanywa kulingana na wakati mgonjwa alibainika kuwa hawezi kulipa ikilinganishwa na wakati malipo ya mgonjwa yalipofanywa. Mgonjwa huweza kurudishiwa pesa kwa ajili ya masalio ya mikopo, kwa sababu ya malipo ya mgonjwa, yanayotokana na idhini zilizotolewa ili kumpa msaada wa kifedha kwa masalio yaliyoangaliwa. Malipo ya kupokea huduma zinazotolewa wakati wa kipindi cha kutathmini ustahiki kwa msaada wa kifedha yatarejeshwa, kama kiasi hicho kinazidi gharama ya mgonjwa kwa \$ 5.00 au zaidi.
10. Wagonjwa ambao wanapata huduma nyingine za matibabu (kwa mfano, bima msingi na ya sekondari au mtoa huduma anayehitajika, anajyejulikana kama carve-out), lazima watumie na kumaliza faida zao kabla ya kutuma ombi kwa Mpango wa Msaada wa Kifedha.

**Matatizo ya kifedha**

Kiasi cha gharama ya matibabu bila bima kinachotozwa katika kituo chochote cha DHS kitazingatiwa katika kuamua ustahiki wa mgonjwa kwa Mpango wa Msaada wa Kifedha. Miongozo ifuatayo imeainishwa kama njia na ya ziada ya kufanya uamuzi wa ziada wa kustahiki kwa Msaada wa Kifedha, unaojulikana kama Msaada kwa Walio na Matatizo ya Kifedha. Msaada kwa Walio na Matatizo ya Kifedha utatolewa kwa wagonjwa wote ambao wameomba Msaada wa Kifedha.

Msaada wa Shida ya Fedha za Matibabu unapatikana kwa wagonjwa ambao kwa njia nyingine hawastahiki kupata Msaada wa Kifedha chini ya miongozo ya msingi ya sera hii, lakini:

- 1) Madeni yao ya gharama za matibabu katika vituo vya DHS yanazidi 25% ya Mapato ya Familia ya kila Mwaka, na hili linasababisha Matatizo ya Kifedha katika kupata Matibabu; na
- 2) ambao wanatimiza viwango vya mapato vya kiwango hiki cha Msaada.

Kwa wagonjwa ambao wanastahiki kwa Gharama za Matibabu Zilizopunguzwa chini ya vigezo vya msingi vya Msaada wa Kifedha na vya Msaada wa Ugumu wa Maisha, DHS itakubali kupunguza gharama ambazo ni mwafaka zaidi kwa mgonjwa kwa ajili ya matibabu ya kiafya ambayo ni muhimu kwa kaya kwa kipindi cha miezi (12), inayozidi 25% ya mapato ya kila mwaka ya familia hiyo.

Madeni ya Matibabu ni gharama za kujilipia mwenyewe kwa gharama zinazopatikana katika matibabu ya lazima ya kiafya.

Mara tu mgonjwa anapoidhinishwa kupata Msaada Kutokana na Shida za Kifedha, bima itaanza kutumika kuanzia mwezi wa tarehe ya kwanza ya kustahiki kwa huduma hadi miezi (12) inayofuata ya kalenda kutoka tarehe ya kukamilishwa kwa tathmini ya maombi. Kila mgonjwa atafanyiwa tathmini kwa kuchunguza kila hali iliyopo ili kubaini muda wa kustahiki kwa mpango, kulingana na kipindi cha ugonjwa/kipindi cha huduma. Bima inashughulikia mgonjwa na wanafamilia wa karibu wanaoishi katika kaya moja, kulipia gharama zilizopunguzwa za matibabu muhimu ya kiafya katika kipindi cha kustahiki kilichowekwa. Bima haitatumika kwa taratibu za zisizo za lazima au za mapambo. Hata hivyo, mgonjwa au mdhamini lazima aijulishe hospitali kuhusu ustahiki wao wakati wa kusajiliwa au kulazwa. Ili kuendelea katika mpango baada ya muda wa kila kipindi cha ustahiki kumalizika, kila mgonjwa lazima awasilishe ombi tena ili kuidhinishwa tena. Pia, wagonjwa walioidhinishwa kwa mpango lazima wafahamishe hospitali kuhusu mabadiliko yoyote ya mapato, mali, gharama au hali ya familia (kaya) ndani ya siku 30 baada ya mabadiliko hayo.

Masharti mengine yote ya kustahiki, kutostahiki na taratibu za msingi za vigezo vya kustahiki kwa mpango wa Msaada wa Kifedha zinatumiwa sawa kwa vigezo vya Msaada Kutokana na Ugumu wa Maisha, isipokuwa katika hali nyingine iliyopo hapo juu.

**Rufaa**

**UTARATIBU, Maendelezo**

- Wagonjwa ambao maombi yao ya msaada wa kifedha yamekataliwa wana chaguo la kukata rufaa dhidi ya uamuzi.
- Rufaa inaweza kuwasilishwa kwa njia ya mdomo au kwa maandishi.
- Wagonjwa wanahimizwa kuwasilisha hati zaidi zitakazotoa sababu madhubuti za kubatilishwa kwa uamuzi wa kunyimwa msaada.
- Rufaa hunakiliwa katika data za mtu wa tatu na katika vyombo vya taratibu hiyo. Kisha zinapitiwa upya na ngazi ya pili ya usimamizi iliyo juu ya mwakilishi ambaye alikataa ombi la awali.
- Kama ngazi ya kwanza ya rufaa haitafaulu katika kubatilisha uamuzi wa kunyimwa msaada, mgonjwa ana fursa ya kupanda katika ngazi nyingine ya usimamizi ili kusikizwa tena.
- Kupanda ngazi huku kunaweza kuendelea hadi kwa Afisa Mkuu wa Fedha atakayetoa uamuzi wa mwisho.
- Barua ya uamuzi wa mwisho itawasilishwa kwa kila mgonjwa liyewasilisha rufaa rasmi.

**Hukumu**

Ikiwa baadaye mgonjwa atabainika kustahiki kupata Msaada wa Kifedha baada ya hukumu kutolewa au deni kuwasilishwa katika shirika la kuripoti mikopo, DHS itabilisha uamuzi wa awali na/au kutupilia mbali taarifa mbaya ya mikopoi.

<b>% Iliyotupiliwa mbali</b>	<b>100%</b>	<b>100%</b>	<b>70%</b>	<b>60%</b>	<b>50%</b>	<b>25%</b>
<b>Ukubwa wa Familia</b>	<b>Mapato</b>	<b>Mapato</b>	<b>Mapato</b>	<b>Mapato</b>	<b>Mapato</b>	<b>Mapato</b>
<b>1</b>	\$12,060	\$24,120	\$27,135	\$30,150	\$36,180	\$60,300
<b>2</b>	\$16,240	\$32,480	\$36,540	\$40,600	\$48,720	\$81,200
<b>3</b>	\$20,420	\$40,840	\$45,945	\$51,050	\$61,260	\$102,100
<b>4</b>	\$24,600	\$49,200	\$55,350	\$61,500	\$73,800	\$123,000
<b>5</b>	\$28,780	\$57,560	\$64,755	\$71,950	\$86,340	\$143,900
<b>6</b>	\$32,960	\$65,920	\$74,160	\$82,400	\$98,880	\$164,800
<b>7</b>	\$37,140	\$74,280	\$83,565	\$92,850	\$111,420	\$185,700
<b>8</b>	\$41,320	\$82,640	\$92,970	\$103,300	\$123,960	\$206,600
Kwa familia/kaya zilizo na watu zaidi ya 8, ongeza \$ 4,180 kwa kila mtu wa ziada.						
<b>% ya Mapato yaliyo katika au juu ya Miongozo ya Umaskini</b>	<b>100%</b>	<b>200%</b>	<b>225%</b>	<b>250%</b>	<b>300%</b>	<b>500%</b>

**UTARATIBU, Maendelezo**

<b>ya 2017</b>						
----------------	--	--	--	--	--	--



